THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

# DARASA LA TANO - KNEB 2021

_PRE - GOLD

# KISWAHILI: LUGHA

*Muda: Saa 1 dakika 40*

*Soma vifungu vifatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Nchini __1__ makabila __2__ mno. Makabila __3__ huhitilafiana sana katika tamaduni zao. Kuna __4__ kuwa tamaduni zao zina ustaarabu mwingi __5__ uliokita mizizi. Jambo la __6__ ni kuwa __7__ tofauti hizi, wote huheshimiana kama wakenya na kila __8__ humuamini mwenziwe. Kutofautiana __9__ tamaduni zao hakujaleta pingamizi __10__ katika harakati zao za kila siku.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | petu mna | kwetu mna | mwetu mna | yetu mna |
| 2. | nyingi | mengi | mingi | haba |
| 3. | hizi | hii | hawa | hiya |
| 4. | wale wanayoshikilia | wale wanaoshikilia | yale yanaoshikilia | zile zinashikilia |
| 5. | na | wa | ya | za |
| 6. | ibura | kawaida | aghalabu | sababu |
| 7. | ingawaje | Licha ya | zaidi ya | kwa ajiliya |
| 8. | mmoja yapo | mmoja kwao | mmoja wao | mmoja wake |
| 9. | kwa | katika | kwenye | na |
| 10. | yoyote | vyovyote | chochote | zozote |

Kutolewa na __11__ kwa elimu ya bure katika shule za msingi kote nchini, kutawawezesha wanagenzi wengi kupata mwangana __12__ na kutoka __13__ giza totoro lililokuwa limetanda nchini. Heko kwa serikali __14__ __15__ ambalo limekuwa kikwazo cha maendeleo ya jamii na nchi.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 11. | kufanikisha | kufenikio | kufanikishwa | kufanikia |
| 12. | kuzindukana | kuzindukiwa | kuzinduka | kuzindusha |
| 13. | kwenye | kati ya | na | kwa |

Ecolebooks.com

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **14.** | A. kutambiza | B. kutambua | C. kutambulisba | D. kutambuliwa |
| **15.** | A. hii janga | **B.** hili janga | C. hiyo janga | D. hizi janga |

O *Stepford Press and Publishers, 2021*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com



Kutoka swali 16 hadi 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.

16. Jana______wali kwa nyama.
    A. tumekula
    B. tulikula
    C. tutakula
    D. tunakula

17. Akisami % huitwa
    A. robo
    B. theluthi
    C. nusu
    D. moja kwanne

**18.** Tumia kivumishi '**-enye**' kwa usahihi:
Nyok____ alinitisha si mkubwa.
    A. wenye
    B. lenye
    C. yenye
    D. mwenye

**19.** Magari _______yameangukamajini.
    A. nyingine
    B jingine
    C. ingine
    D. mengine

**20.** Hili ni umbo lipi?
    A. **Pia**
    B. Mche
    C. Duara dufu
    D. Pembe tatu

**21.** Kamilisha methali ifuatayo:
Damu ni nzito kuliko.
    A. maji
    B. moto
    C. mfupa
    D. nyama

23. Jibu maamkizi yafuatayo:
Salaam aleikum
    A. sijambo
    B. aleikm salaam
    C. marahaba
    D. asante

24. Andika tarakimu 77,777 kwa maneno
    A. Elfu mia saba sabini na saba na sabini na saba.
    B. Elfu sabini na saba, mia saba sabini na saba.
    C. Elfu sabini mia saba sabini na saba.
    D. Elfu saba na sabini na saba.

25. Turia -ote kwa usahihi:
Nguo _______ zitaoshwa
    A. wote
    B. lote
    C. yote
    D. zote

22. Msemo 'kupiga mguu' maana yake ni
    A. kulalia miguu
    B. kucheza uwanjani
    C. kwenda kasi
    D. kutembea kwa miguu

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM


26. Jaza pengo kwa usahihi;
Sijamwona Yusu ___ jana.
A. tangu
B. kama
C. mpaka
D. toka

27. Tegua kitendawili kifuatacho: Miti yangu haipandiki
A. Nyasi
B. Macho
C. Sufuria
D. Shimo

28. Andika wingi wa:
Mtoto mzuri amepata zawadi.
A. Vitoto vizuri vimepata mazawadi.
B. Watoto wazuri wamepata zawadi.
C. Watoto mzuri wamepata zawadi.
D. Mtoto wazuri wamepata zawadi.

29. Kanusha: Mti imeanguka.
A. Miti haijaanguka.
B. Miti haik~anguka.
C. Miti haikuanguka.
D. Miti baianguki.

30. Mtoto wa mtoto wangu ni
A. mjukuu
B. kitukuu
C. shemeji
D. mpwa



Ecolebooks.com



*Soma ufcham ufuatao kisha ujibu maswali* 31 - **40**.

Uhasama dhidi ya simba na ng'ombe ulianza zama za kale kabla ulimwengu haujapata maarifa tuliyo nayo hivi leo. Wagombanao ndio wapatanao ni methali ambayo haikusadifu wala kufua dafu kati ya hao sahibu wawili kwani baada ya ugomvi wao, walitengana kama ardhi na mbingu mpaka leo, kamwe hawapikiki katika chungu kimoja.

Siku moja, ndama na mwanasimba walikuwa wakicheza pamoja kwa furaha na bashasha. Wazazi walikwenda kuwinda lakini katika zile hekaheka za kucheza pamoja, ukazuka mkasa bin mkosi uliozaa balaa bin belua. Mwanang'ombe alimdunga mwanasimba kwa pembe. Ilikuwa ni ajali na ajali haina kinga wala kafara.

Alasiri ilipowadia, wazazi walirejea chengoni na kumkuta mwanasimba machozi kupukupu naye mwanang'ombe tumbo moto. Bila simile, mama simba akapashwa habari na mwanasimba. Wacha achemke nyongo, wacha pazuke taharuki na mtafaruku. Ng'ombe na mwanawe pale hapakuwafaa tena Damu ina mzizimo wa kondoo mwenye manyoya haba. Alipopima uwezo wake mbele ya malkia wa wanyama, ng'ombe wakatundika maguu mabegani na kuch~na mbuga. Haaoo! Wakatokomea hadi maskanim kwa binadamu kutafuta stara, nako ndiko aishiko mpaka leo.

**31.** Uhasama dhidi ya simba na ng'ombe ulianza
- A. siku zijazo
- B. kitambo
- C. siku za usoni
- D. hizi majuzi

**32.** Kwanini ngombe na simba walitengana kama ardhi na mbingu? Kwa sababu ya
- A. umaskini mwingi.
- B. urafiki mkubwa.
- C. upendo wa dhati.
- D. ugomvi kati yao.

**33.** Nini kilichofanyikia wazazi walipoenda kuwinda?
- A. Mwanang'ombe alimdunga mwanasimba kwa pembe.
- B. Mwanang'ombe alimuua mwanasimba.
- C. Mwanasimba alimuua mwanang'ombe.
- D. Walipatwa na bahati mbaya ya maafa.

**34.** Wazazi walirejea nyumbani wakati upi?
- A. Usiku
- B. Alasiri
- C. Adhuhuri
- D. Asubuhi

**35.** Simba alipashwa habari zilizotokea na?
- A. Ng'ombe
- B. Ndama
- C. Jirani
- D. Mwanawe

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

36. Ni kweli kusema kuwa
A. urafiki wa simba na ng'ombe ulidumu.
B. simba alimuua ng'ombe.
C. urafiki wa ng'ombe na simba uliisha.
D. ng'ombe na mwanawe walizua uadui na binadamu.

37. Maana ya semi 'chemka nyongo' kulingana na taarifa ni
A. changanyikiwa
B. patwa na wasiwasi.
C. furahi.
D. kasirika.

38. Ng'ombe na mwanawe walitorokea wapi?
A. Vichakani
B. Majini
C. Msituni
D. Kwa binadamu

39. Simba ameitwa malkia wa wanyama, kuonyesha kuwa
A. yeye ni hakimu wa wanyama.
B. yeye ni kiongozi wa wanyama.
C. yeye ni mama wa wanyama.
D. ycye ni mlinzi wa wanyama.

40. Maana ya methali 'Ajali haina kinga wala kafara' kama ilivyotumika katika taarifa ni
A. huwezi kuzuia ajali.
B. usipojikinga utatoa kafara.
C. unaweza kuzuia ajali.
D. ajali ina kinga.

Ecolebooks.com



*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Viazi ni aina ya vyakula vya mizizi. Kimoja ni kiazi. Kuna aina nyingi za viazi. Kwanza, ni viazi vitamu. Hivi huliwa sana katika nchi za joto kama hizi zetu za Afrika ya Mashariki. Vazi vyenyewe ni vitamu vivyo hivyo vinavyoitwa.

Viazi vitamu huliwa kwa kupikwa au kuchemshwa. Pia, huweza kugegetwa ama kutafuwa bila kupikwa. Upishi maarufu wa viazi ni kukokoswa. Yaani, butiwa chunguni au sufuriani, kisha kutiwa maji kiasi cha kutosha.

Huchemshwa kwa muda hadi ngozi yake ilainike kama samli. Chungu huepuliwa kisha viazi hupakuliwa na kuachwa vipigwe na upepo. Viazi hivyo huweza kuliwa kwa kitoweo chochote kama vile nyama, samaki, mboga au mchuzi. Pia, huweza kutafuniwa vizuri na kinywaji kama chai, uji au maziwa.

Aina nyingine ya viazi ni **yugwa** au jimbi. Pia, huitwa viazi vikuu. Hupikwa kwa kutokoswa kwenye maji au matuta lakini huwezi kukigegata kikiwa kibichi. Viazi vingine ni mbatata. Wengine huviita viazi viviringo au kiazi ulaya. Hivi havina ladha yoyote tamu lakini vinaliwa sana, tena kwa namna nyingi mno. Kwanza ni katika kitoweo chochote kama vile nyama, samaki au mboga Huunga supu vizuri sana. Hutokoswa kwa kutiwa chumvi na mafuta na kuwa kitoweo. Aidha, hukatwa vipande bapa kama **silesi** ya mkate na kutengenezwa, kaukau, krisol kwa kimombo. Mapishi mengine ya mabatata ni kukatwakatwa mifano ya vidole na kukaangwa kwenye mafuta mengi. Baada ya kuiva, hutolewa kutoka kwa mafuta hayo mengi na hupakuliwa kwenye vijisahani ambapo baada ya kurashiarashia chumvi, nyanya na asali, huwa chakula kitamu kupindukia. Hiki ndicho chakula maalum walaji wa siku hizi mjini wamezoea.

Karoti ni aina nyingine ya kiazi. Zenyewe hutumika kama kiungo cha kachumbari, mchuzi ama huliwa mbichi. Viazi vitamu vinaweza kupandwa kwenye vichuguu, matuta au wa njia kawaida ya kilimo cha sasa. Yugwa hulimwa mahali penye tope au penye maji mengi sana. Mbatata hupandwa mahali popote mradi pawe na mvua ya kutosha. Viazi vitamu ni chakula cha kuongeza nguvu mwilini. Majani ya mihogo yanaitwa **kisamavu.**

**41.** Katika taarifa hii, vimetajwa viazi aina ngapi?

A. Sita B. Tano
C. Tatu D. Nne

42. Aina maarufu ya upishi wa viazi karibu vyote ni

A. kutokoswa B. kukaangwa
C. kugegetwa D. kuchemshwa

**46.** Vichuguu, matuta au sesa vinaweza kutumika kwa upanzi wa

A. karoti B. viazi vitamu.
C. mbatata D. yugwa

47. Kisamvu ni majani ya

A. mipera B. mahindi
C. mgomba D. mihogo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

43. Viazi vinavyostawi mahali penye tope kaitwa

A. mabati B. karoti
C. yugwa D. viazi vitamu

44. Kaukau pia huweza kuitwa
A. kripi B. viazi
C. mandondo D. vibanzi

45. Viazi vitamu huongeza
A vitamini B. nguvu
C maji D. madini

48. Viazi vyote ni vyakula vya
A. majani B.matunda
C. nafaka D.mizizi

49. Anayefanya kazi ya ukulima huitwa
A. mkalimani B. mkulima
C. mtafiti D. mlimi

50. Taarifa hii inafaa kichwa gani bora?
A. karoti B. Viazi
C. Yugwa D.Chakula

© Stepford Press and Publishers 2021